


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

MAADHIMISHO YA WIKI YA AFYA KITAIFA – 2025

TAREHE 3 – 8 APRILI, 2025

**KITABU CHA MAWASILISHO YA MDAHALO WA WAZI KWA UMMA
UNAOFANYIKA TAREHE 4 APRILI, 2025**

&

**DARASA HURU KWA UMMA LINALOFANYIKA TAREHE
5-7 APRILI 2025 KWA NJIA YA MTANDAO**

KITUO CHA MIKUTANO CHA JAKAYA KIKWETE – DODOMA


TULIPOTOKA, TULIPO, TUNAPOELEKEA: TUNAJENGA TAIFA LENYE AFYA



**World Health
Organization**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

MAADHIMISHO YA WIKI YA AFYA KITAIFA – 2025

TAREHE 3 – 8 APRILI, 2025

KITUO CHA MIKUTANO CHA JAKAYA KIKWETE – DODOMA

**KITABU CHA MAWASILISHO YA MDAHALO WA WAZI KWA UMMA
“SYMPOSIUM” UNAOFANYIKA TAREHE 4 APRILI, 2025**

&

**DARASA HURU “MASTER CLASS” KWA UMMA LINALOFANYIKA TAREHE
5-7 APRILI 2025 KWA NJIA YA MTANDAO**

MADA YA MDAHALO WA WAZI “SYMPOSIUM”

TULIPOTOKA, TULIPO, TUNAPOELEKEA: TUNAJENGA TAIFA LENYE AFYA

Kamati ya Maandalizi ya Mdahalo wa Wazi “Symposium”

Mwenyekiti: Tumainiel Macha

Katibu: Simon Nzilibili – MoH

Wajumbe: Dkt. Otilia Gowelle – MoH
Dkt. Ona Machangu – MoH
Dkt. Elizabeth Shayo – NIMR
Dk. Vivian Wonanji – MoH
Dkt. Emmanuel Mkeni – MoH
Asnath Mpelo – MoH
John Yuda – MoH
Dkt. Norman Jonas – MoH
Dkt. Chacha Mangu – MoH
Dkt. Pius Kagoma – OR - TAMISEMI
Prof. Stephen Kibusi – UDOM
Dkt. Shakilu Jumanne - UDOM
Dkt. Witness Mchwampaka
Dkt. James Kengia – OR-TAMISEMI
Dkt. Golden Masika – UDOM

WIZARA YA AFYA

MAADHIMISHO YA WIKI YA AFYA KITAIFA

MWAKA 2025



MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB)
WAZIRI WA AFYA



Dkt. GODWIN O. MOLLEL (MB)
NAIBU WAZIRI WA AFYA



Dkt. SEIF A. SHEKALAGHE
KATIBU MKUU



ISMAIL H. RUMATILA
NAIBU KATIBU MKUU

Foreword



As the Chief Medical Officer, I am delighted to provide foreword in this important document that outlines key presentations with research evidence and innovation for improving the health of Tanzanians. The Tanzanian Government through the Ministry of Health and the global universe has been commemorating the World Health Day which usually takes place on 7th April each year. The event serves to raise awareness about critical health issues, recognize health workers' contributions, and advance discussions on effective health promotion strategies. Having recognized the importance of making informed decision making and advancement in science and technology in care and treatment, the Ministry of Health has organized **a one-day** Symposium aiming at sharing significant research evidence for improving the health and welfare to Tanzanians. The symposium serves as a platform for dialogue, exchange, and knowledge sharing among different stakeholders. During the symposium, health practitioners, policymakers, researchers, implementing and development partners, diaspora and academia come together to discuss and deliberate on best practices, groundbreaking evidence, and innovative solutions that demonstrate the immense potential of improving the health of Tanzanians.

As part of a week-long commemoration of National Health Week, the theme of this year is 'Tulipotoka, Tulipo, Tunapoelekea: Tunajenga Taifa Lenye Afya'. This theme reflects the historical background, the shortfalls, strengths, opportunities and progress we have achieved so far through targeted interventions in key priority areas of concern as per Sustainable Development Goals. The symposium has three subthemes as follows:

- i. **Advancement in Healthcare Service Delivery**
- ii. **Integrated Health Services Delivery**
- iii. The role of research evidence in improving the health of Tanzanians

During this symposium, a total of nine presentations will be made reflecting important board areas of research and innovations. This will be preceded with a **keynote address** focusing on the role of research in improving the health of all Tanzanians. Each thematic area will be summed up with a panel discussion on key issues emanated and deliberations. Thus, this Symposium provides opportunities for strengthening collaboration between health practitioners, researchers, academia, and local and international organizations in commemorating International Health Day.

As a Chief Medical Officer, I look forward to the interactive sessions, through sharing experiences and learnings in the presentations and discussions as the ultimate goal is to improve the health of Tanzanians. Welcome All.

Dr. Grace Magembe
CHIEF MEDICAL OFFICER – MOH

PROGRAMU YA MDAHALO

SHEREHE ZA UFUNGUZI

Mwezeshaji: Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya – Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili - MOI

Muda	Tukio	Mhusika
01:30 - 02:25	Washiriki kuwasili na kujisajili	Kamati ya Ukaribisho
02:25 - 02:30	Mgeni Rasmi kuwasili	Mwenyekiti wa Maadhimisho
02:30 - 02:35	Wimbo wa Taifa	Kamati ya Itifaki
02:35 - 02:40	Utangulizi na utambulisho	Mwenyekiti wa Kamati ya Mdahalo
02:40 - 02:45	Neno la ukaribisho	Mganga Mkuu wa Serikali
02:45 - 02:50	Salam kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma	Prof. Lughano Jeremy Kusiluka - UDOM
02:50 - 03:05	<i>WHO remarks on Ending Preventable Maternal Mortality (EPMM) and Every New Born Action Plan (ENAP)</i>	Dkt. Edwin Swai - WHO
03:05 - 03:35	Wasilisho Kuu "KeyNote": Matumizi ya tafiti katika kuboresha Afya kwa wote nchini	Prof. Said Aboud-NIMR
03:35 - 03:50	Ufunguzi wa Mdahalo	Mhe. Jenista Muhagama - Waziri wa Afya
03:50 - 03:55	Neno la shukrani	Naibu Katibu Mkuu OR-TAMISEMI
03:55 - 03:00	Picha kwa makundi yaliyoandaliwa	GCU-MoH
03:00 - 04:30	CHAI	WOTE

MADA 1: UBORESHAJI WA UTOAJI WA HUDUMA BOBEZI ZA AFYA NCHINI

Mwenyekiti: Prof Abel Makubi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamini Mkapa - BMH

Watunza Kumbukumbu: John Yuda, MoH na Dkt. Chrisogone German, MoH

Muda	Mawasilisho yatakatayofanyika	Wawasilishaji
04:30 - 04:55	Matumizi ya sayansi katika kuboresha huduma za Figo: Uchujaji wa Damu na Upandikizaji wa Figo nchini	Profesa Masumbuko Mwashambwa - UDOM
04:55 - 05:20	Matumizi ya sayansi katika kuboresha utoaji wa huduma bobezi za upandikizaji wa Uloto kwa Watoto wenye magonjwa ya Damu na Saratani	Dkt. Shakilu Jumanne - UDOM
05:20 - 05:45	Matumizi ya teknolojia katika ufanisi wa matibabu ya magonjwa ya moyo nchini	Dkt. Angela Muhozya - JKCI
05:45 - 06:15	Maswali na Majadiliano	Prof. Stephen Kibusi - UDOM

MADA 2: UTOAJI WA HUDUMA JUMUISHI ZA AFYA

Mwenyekiti: Prof Kawshik Ramaiya, Katibu Mkuu wa TANCDA na TDA Tanzania

Watunza Kumbukumbu: Dkt. Clarer Jones, MoH na Dkt. Mercy Chiduo, NIMR

Muda	Mawasilisho yatakayofanyika	Wawasilishaji
06:15 - 06:40	Huduma jumuishi za Tiba Asili katika Hospitali za Rufaa za Mikoa Tanzania	Dkt. Winifrida Kidima - MoH
06:40 - 07:05	Mchango wa Huduma jumuishi za Afya Ngazi ya Jamii katika kuwezesha huduma za Afya kwa Wote	Dkt. Norman Kyala - MoH
07:05 - 07:30	Mwenendo wa Magonjwa Yasiyo ambukiza na Viashiria vyake nchini (STEP SURVEY)	Dkt. Mary Mayige wa NIMR na Dkt. Ubuguyu wa MoH
07:30 - 08:00	Maswali na Majadiliano	Dkt. Paul Kazyoba - NIMR
08:00 - 09:00	CHAKULA CHA MCHANA	WOTE

MADA 3: TAFITI NA MABORESHO KATIKA SEKTA YA AFYA TANZANIA

Mwenyekiti: Dkt. Basiliana Emidi, Meneja na Afisa Tafiti Mkuu kutoka Taasisi ya Tafiti za Binadamu - NIMR

Watunza Kumbukumbu: Dr Nura, FELTEP, Dr Caroline DCS

Muda	Mawasilisho yatakayofanyika	Wawasilishaji
09:00 - 09:25	Umuhimu wa 'Afya moja' katika kudhibiti magonjwa ya milipuko nchini	Dkt. Chacha Mangu - MoH
09:25 - 09:50	Maoni ya Wana-Diaspora juu ya Huduma za Afya Nchini	Prof. Gideon Mlawa – TUHEDA UK
09:50 - 10:20	Historia na Maboresho ya sekta ya Afya Tanzania kuelekea kuwa na Afya kwa Wote.	Dkt. Ntuli Kapologwe - MoH
10:20 - 10:50	Maswali na Majadiliano	Dkt. Leonard Subi – Kibong'oto

SHEREHE ZA HITIMISHO LA MDAHALO

Mwezeshaji: Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya – Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili - MOI

Muda	Tukio	Mhusika
10:50 - 10:55	Mgeni Rasmi kuwasili	Mwenyekiti wa Maadhimisho
10:55 - 11:00	Maoni na Maazimio ya Mdahalo	Mwenyekiti wa Mdahalo
11:00 - 11:05	Kumkaribisha Mgeni Rasmi	Mganga Mkuu wa Serikali
11:05 - 11:20	Kufunga Mdahalo	Katibu Mkuu – MoH

Wasilisho Kuu

Wasilisho: Matumizi ya tafiti katika kuboresha Afya kwa wote nchini

Jina: Prof. Said S. Aboud; MD, MPhil, MMed, PhD

Cheo: Mkurugenzi Mkuu

Taasisi: Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

Barua pepe: said.aboud@nimr.or.tz

Katika miongo kadhaa iliyopita, Tanzania imepiga hatua kubwa kuelekea kufikia ajenda ya afya kwa wote kwa kuimarisha mifumo ya afya, kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu za afya na kukuza ufahamu wa afya kupitia juhudi shirikishi. Wizara ya Afya imesisitiza umuhimu wa kutumia njia mbalimbali za kuimarisha afya za watazania ambazo "zimetokana na kuongozwa na shahidi za kitafiti zilizotengenezwa nchini Tanzania" ili kuhakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma.

Katika muktadha huu Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), chini ya Wizara ya Afya, ina jukumu la kuratibu, kukuza utafiti na kutafsiri matumizi yake katika kuboresha Sekta ya Afya na utoaji wa huduma za afya za kila siku nchini. Kujikita katika mbinu za kitafiti zimeleta maendeleo makubwa katika kufikia malengo ya mfumo wa Afya kuanzia kwenye utoaji wa huduma, utawala bora, ushirikishwaji wa Wadau katika kuongeza usawa wa utoaji wa huduma za Afya nchini Tanzania. Uchambuzi huu unaonesha mafanikio yaliyofikiwa hapo juu ukisisitiza hitaji la uvumbuzi zaidi katika sekta ya afya.

Kwa kutumia takwimu za Tanzania na kusoma/kuelewa machapisho ya kiafya, Taasisi inaangalia namna ambavyo Mikakati iliyotumia shahidi za Kisayansi zilivyoboresha huduma za afya, uwezo wa wafanyakazi wa afya, mifumo ya habari, upatikanaji wa dawa kwa watumiaji, ufadhili katika sekta ya afya, pamoja na uongozi / utawala/ usimamizi bora katika kuendeleza afya kwa wote.

Keynote Speech

Title: *The role of research in advancing health for all in Tanzania*

Name: *Prof. Said S. Aboud MD, MPhil, MMed, PhD*

Position: *Executive Director*

Institution: *National Institute for Medical Research*

Email: said.aboud@nimr.or.tz

During the past decades, Tanzania has made significant strides towards achieving the health-for-all agenda by strengthening health systems, improving access to essential healthcare services and promoting awareness through collaborative efforts.

The Ministry of Health has emphasised the importance of interventions that are "inspired and guided by locally generated evidence" to ensure no one is left behind. In this context the National Institute for Medical Research (NIMR), under the Ministry of Health, plays a pivotal role in coordinating research and translating findings into health policy and practice.

This commitment to an evidence-based approach has driven significant progress in achieving key health system targets, spanning service delivery, governance, and stakeholder engagement to enhance health equity in Tanzania. This analysis reflects on past achievements while underscoring the need for further research-driven innovations in the health sector.

Using Tanzanian data and case studies, it examines how evidence-based initiatives have strengthened health services, workforce capacity, information systems, access to medicines, health financing, and leadership/governance in advancing health for all.

MADA 1: UBORESHAJI WA UTOAJI WA HUDUMA BOBEZI ZA AFYA NCHINI

Mwenyekiti/Chairperson: Prof. Abel N. Makubi
MD, MMed (Int.med), MSc (Haem), Dip Card, PhD (Card), FRC, FESC

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa na Katibu Mkuu Mustaaifu wa Wizara ya Afya (*Executive Director of Benjamin Mkapa Hospital and former Permanent Secretary (PS) of the Ministry of Health*)

Wasilisho: Matumizi ya Sayansi Katika Kuboresha Huduma za Figo; Tulipotoka, Tulipo na Tunapokwenda Katika Uchujaji Damu na Upandikizaji Figo Tanzania

Jina: Prof. Masumbuko Yatembela Mwashambwa

Cheo: Professor Idara ya Upasuaji

Taasisi: Chuo Kikuu cha Dodoma

Barua pepe: Masumbuko.mwashambwa@udom.ac.tz.

Utangulizi na Umuhimu: Magonjwa ya figo ni tatizo kubwa la kiafya duniani, yakikadiriwa kuathiri watu milioni 850 (10% ya watu wote) mwaka 2019, ikilinganishwa na milioni 422 wenye kisukari, milioni 42 wenye saratani, na milioni 36.7 wenye VVU. Takriban watu milioni 1.4 hufariki kila mwaka, sawa na 2.4% ya vifo duniani, vingi vikitokea kwenye nchi maskini. Kwa ujumla inakadiriwa kuwa asilimia 4.5 hadi 13 ya watu duniani wana matatizo ya figo, Africa ndiyo yenye idadi ndogo. Aidha, zaidi ya 75% ya visa vya figo kushindwa kwa ghafla (AKI) hutokea katika jamii, ambapo takriban watu milioni 13.5 huathirika kila mwaka.)

Malengo: Kuchambua hali ya sasa ya huduma za figo nchini Tanzania, ikijumuisha uchujaji damu na upandikizaji figo, pamoja na mafanikio, changamoto, na maeneo ya maboresho.

Mbinu na Taratibu zilizotumika: Taarifa zimekusanywa kupitia mapitio ya nyaraka za kitaifa kuhusu huduma za dialysis, machapisho na kumbukumbu za wagonjwa waaliopandikizwa figo

Matokeo: Huduma za figo nchini zimeimarika kwa kasi. Takriban wagonjwa 3327 wanapata huduma za hemodialysis kote nchini, kutoka kwenye vituo zaidi ya 24 vya umma vilivyowekewa mashine 597 za kisasa. Huduma za upandikizaji figo zimeanzishwa katika MNH, Mloganzila, na BMH, ambapo jumla ya wagonjwa 151 wamepandikizwa figo: 89 MNH Upanga, 12 Mloganzila na 50 BMH. Kati ya hawa, 86-90% wanaendelea vizuri, 16% walipata matatizo madogomadogo, na 7-14% walifariki. Mafanikio haya yametokana na uwekezaji katika miundombinu, ununuzi wa vifaa vya kisasa, mafunzo kwa wataalamu, na ushirikiano wa kimataifa.

Hitimisho na Ushauri: Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuboresha huduma za figo, ikiwemo kufanikisha upandikizaji figo ndani ya muda mfupi hatua ambayo haijafikiwa na nchi nyingi za Afrika. Pamoja na changamoto zilizopo, msingi wa

mafanikio upo na unaonyesha matumaini makubwa ya kuendeleza huduma hizi kwa ufanisi zaidi.

Title: *The use of science in improving kidney services in Tanzania; past, present and future of hemodialysis and kidney transplant services*

Name: Prof. Masumbuko Yatembele Mwashambwa

Position: Associate Professor of Surgery

Institution: University of Dodoma

Email: Masumbuko.mwashambwa@udom.ac.tz

Introduction: *Kidney diseases are a major health burden worldwide. In 2019 850 million people (10% of population) were affected. This was twice as much as Diabetes mellitus (422 million), twenty times to all cancers (42 million) and HIV/AIDS (36.7 million). Approximately 1.4 million people die annually (2.4% of all causes of deaths), most occur in the lower- and middle-income countries. An actual prevalence varies, ranging from 4.5 to 13%, with Africa having the lowest. Furthermore, there are about 13.5 million cases of acute kidney injury, the majority (75%) from the community. Tanzania started renal service less than two decades, this analysis aims to put forward current situation and way forward.*

Main objective: *To analyze existing kidney services provision in Tanzania; hemodialysis and kidney transplant, record success, challenges and areas of improvement.*

Methodology: *Review of articles, patients' records and reports from various stakeholders, including the Ministry of Health.*

Results: *Kidney services in the country have rapidly expanded. In Tanzania there are 3327 patients on hemodialysis, from 24 hemodialysis centers with 597 hemodialysis machines. Kidney transplant (KT) services are offered at Muhimbili National Hospital (Upanga and Mloganzila) and Benjamin Mkapa Hospital in Dodoma. One hundred and fifty-one cases have undergone KT (89 MNH Upanga, 12 Mloganzila and 50 BMH). Of these cases 86-90% are well, 16% had minor complications and 7-14% died due to various reasons. Investment in infrastructure, availability of medicines and equipment, human resource training and international collaboration were the main pillars of success. A key challenge is lack of donors.*

Conclusion: *Tanzania has taken a significant leap in initiating kidney services. Despite challenges, KT services in particular, took the shortest time after initiation of hemodialysis services, many African countries are still struggling. With this good beginning, continued improvement will perfect kidney service in the country.*

Wasilisho: Matumizi ya Sayansi kuleta Mageuzi katika matibabu ya Magonjwa ya Damu na Saratani kwa Watoto - Uzoefu kutoka Mradi wa Upandikizaji Uloto Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma

Jina: Dr. Shakilu Kayungo Jumanne

Cheo: Muhadhiri Mwandamizi na Kaimu Amidi wa Shule kuu ya Tiba na Afya ya Kinywa

Taasisi: Chuo Kikuu cha Dodoma

Barua pepe: Shakilu.jumanne@udom.ac.tz

Utangulizi na Umuhimu: Upandikizaji uloto “BMT” kama tiba ya magonjwa ilitumika mara ya kwanza mwaka 1960 huko nchini Marekani na imeendelea kuwa tiba bobeezi kwa magonjwa ya damu na saratani. Matumizi ya tiba hii katika nchi zinazoendelea hasa barani Afrika yamekuwa yakitiliwa shaka hasa kutokana na wasiwasi juu ya usalama wake, gharama kubwa na uwepo wa matitizo mengine mengi makubwa ya kiafya yanayohitaji tiba pia. Mwaka 2023, Tanzania iliingia kwenye orodha ya nchi sita barani Afrika kuanzisha tiba ya upandikizaji uloto kwa watoto wenye ugonjwa wa Siko Seli (Seli mundu). Matibabu haya yalianzishwa katika hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kushirikiana na Chuo kikuu cha Dodoma, na Shirikia la kiitaliano litwalo Help3

Malengo: Kutathmini uwezo na matokeo ya awali ya matibabu ya Upandikizaji uloto kwa watoto ishirini(20) wenye ugonjwa wa Siko Seli katika hospitali ya Benjamin Mkapa

Mbinu na Taratibu zilizotumika: Hatua za maandalizi za kutoa tiba hii zilianza mwaka 2018 zikihusisha maeneo makuu mawili,(1) kuboresha miundo mbinu ya hospitali kukidhi vigezo vya upandikizaji uloto (ikiwemo kuboresha wodi maalum, huduma za uchunguzi na upatikanaji wa damu salama), (2). Kutoa mafunzo kwa timu ya upandikizaji uloto ikijumuisha wataalam mbali mbali. Wodi maalum iliandaliwa, vifaa kwa ajili ya vipimo maalum pamoja na vitendanishi vilinunuliwa na jumla ya watoa huduma 10 walipata mafunzo mahsusi kuhusu tiba hii. Mgonjwa wa kwanza alipatiwa tiba ya upandikizaji uloto kuanzia mwezi Februari, 2023 kwa kutumia miongozo maalum ya matibabu kuhakikisha usalama wa mgonjwa na tiba ya ugonjwa wa Sikoseli.

Matokeo: Kuanzia mwezi Februari, 2023 hadi Machi, 2025, jumla ya wagonjwa 20 (13 wa kiume, 7 wakike)wenye wastani wa umri wa miaka 8 walipata tiba ya upandikizaji uloto. Wote walionyesha dalili za uloto kuota na kuondosha ugonjwa wa Siko Seli ambapo chembe sahani na chembe nyeupe za damu (kama viashiria vya kupona) zilifikia kiwango cha kuridhisha kuanzia siku ya 20 na 28 kutoka siku ya kupandikizwa uloto. Wagonjwa wote 20 walihimili matibabu haya bila shida yoyote kubwa na kupata maudhi kidogo kutokana na matibabu ambayo yalidhibitiwa kwa tiba. Mpaka kufikia mwezi Machi, ikiwa ni wastani wa siku 326 tangu kupandikizwa uloto kwa wagonjwa wote 20, hakuna mgonjwa yoyote alieonyesha dalili za ugonjwa wa Sikoseli na 7 kati yao hawakuwa kwenye matibabu yoyote. Wastani wa gharama za tiba hii unakadiriwa kuwa shilingi milioni 60 (55-75) kutegemea muda wa tiba mgonjwa atakao tumia.

Hitimisho na Ushauri: Matokeo ya mradi huu yameonyesha kuwa tiba ya upandikizaji uloto inaweza kutolewa hapa Tanzania kwa usalama mkubwa kwa kuwa na kitengo maalum na wataalam husika. Gharama za tiba hii ni kubwa kwa mtu mwenye kipato cha kawaida kumudu lakini ni nafuu sana tiba hii kuanyika hapa nchini ukilinganisha na kupata tiba hii nchi za nje. Gharama za tiba hii ambayo huondosha ugonjwa kabisa ni nafuu ukilinganisha na tiba za kawaida za kupunguza makali ambazo mgonjwa hutumia kwa maisha yake yote.

Title: Transforming Care for Childhood Cancer and Blood Disorders through Advancement in Science – Experience from Benjamin Mkapa Hospital Bone Marrow Transplantation Program

Name: Dr. Shakilu Kayungu Jumanne

Position: Senior Lecturer and Acting Dean of the School of Medicine and Dentistry

Institution: University of Dodoma

Email: Shakilu.jumanne@udom.ac.tz

Introduction and rationale: Bone marrow transplantation (BMT), also known as Hematopoietic Stem Cell Transplantation (HSCT) was first used as a curative option in 1960 and has since been a standard of care rescue therapy for several benign and malignant disorders in high-income settings. However, the feasibility of HSCT in LMICs is often questioned over safety concerns, high costs, and presence of other competing health priorities. In 2023, Tanzania became the 6th African country to establish a matched sibling donor allogeneic HSCT for Sickle cell disease in a collaborative project involving Benjamin Mkapa Hospital, the University of Dodoma, and an Italian charity – Help3 Onlus

Objective(s): To evaluate the feasibility and treatment outcomes of the first 20 HSCT cases conducted in Dodoma.

Methodology/Approach: The preparatory phase started in 2018, with a focus on two key priority areas: upgrading the hospital infrastructure (special ward, diagnostic services, and blood bank) to meet minimum HSCT standards and training a multidisciplinary team of experts. A specialized ward was renovated and installed with essential HSCT requirements, an initial team of 10 staff underwent an intensive training program and procurement of required laboratory and blood bank equipment and reagents. The first case was transplanted in February 2023 using a myeloablative conditioning regimen including Busulfan, Rabbit Antithymocyte Globulin, and Cyclophosphamide, with bone marrow as the stem cell source from HLA-matched sibling donors. Methotrexate and cyclosporine were used for GVHD prophylaxis, while Levetiracetam, Acyclovir, Bactrim, and fluconazole were used as prophylactic antimicrobials.

Results: Between February 2023 and March 2025, 20 patients (13 males, 7 females; median age 8 years) underwent HSCT. Nine-teen achieved complete engraftment (median ANC: day +28, PLT: day +20) with manageable HSCT-related complications, including febrile neutropenia episodes, mucositis, grade 2 aGVHD (CTCAv5), and other infections (1 fungal, 1 HPV, 1 Falciparum malaria). Bacterial isolates during febrile neutropenia included Coagulase-negative Staphylococci and Pseudomonas/Acinetobacter species all controlled by course of antibiotic therapy. At a median follow-up of +326(24-786) days, all patients remained SCD symptom-free, with 7 completing immunosuppressive therapy. Average cost: 60M TZS (range: 55–75M) depending on complications acquired

Conclusions & Recommendations: Bone marrow transplantation is a feasible therapy to pursue in Tanzania when performed at a dedicated center by a trained team. The cost of the procedure can be prohibitive for out-of-pocket payments but is much lower than any overseas option. Conventional supportive SCD care, in the long term, is equally expensive compared to HSCT which is a curative option.

Wasilisho: Matumizi ya teknolojia katika ufanisi wa matibabu ya magonjwa ya moyo nchini

Jina: Dr Angela Paul Muhozya (MD, MMED, FCVA).

Cheo: Daktari Bingwa Mbobezi wa Usingizi wa Moyo na Mkurugenzi wa Upasuaji wa Moyo

Taasisi: Taasisi ya Magonjwa ya Moyo ya Jakaya Kikwete

Barua pepe: angela.muhozya@jkci.or.tz

Utangulizi na Umuhimu: Maendeleo ya teknolojia katika matibabu ya moyo

Malengo: Teknolojia ilivyoboresha na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za moyo

Mbinu na Taratibu zilizotumika: Uhakiki wa taarifa, mahojiano, teknolojia zinazotumika kwa sasa.

Matokeo: Kuboresha huduma za matibabu ya moyo nchini

Hitimisho na Ushauri: Wizara ya afya chini ya uongozi wa serekali ya awamu ya sita umewekeza kwa kiwango kikubwa katika teknolojia iliyoboresha ubora lakini pia kutanua uwigo na upatikanaji wa huduma za matibabu ya moyo nchini

Title: *Technology use in expansion and advancement of cardiovascular interventions in Tanzania*

Name: *Dr Angela Paul Muhozya (MD, MMED, FCVA).*

Position: *Consultant Cardiovascular Anaesthesiologist and Director of Cardiac Surgery*

Institution: *Jakaya Kikwete Cardiac Institute*

Email: angela.muhozya@jkci.or.tz

Background/Introduction and rationale: *Technology advancing cardiovascular interventions.*

Objective: *Technology advancement contributing to more accessible and quality cardiovascular interventions*

Methodology/Approach: *Review of current work from JKCI, client's data collected and expert's work contributions.*

Results: *Advancing cardiovascular interventions in Tanzania*

Conclusions & Recommendations: *Ministry of health under the current government leadership has invested extensively in advanced technology of prevention, treatment and management of cardiovascular diseases. This has resulted in accessible but also topnotch cardiovascular interventions of international standards.*

Mwongoza Majadiliano na Maswali: Prof. Stephen Kibusi

Profesa wa Afya ya Jamii na Mkuu wa Shule Kuu ya Uuguzi na Afya ya Jamii katika Chuo Kikuu cha Dodoma
(Associate Professor of Public Health the Dean of School of Nursing and Public Health at the University of Dodoma)

MADA 2: UTOAJI WA HUDUMA JUMUISHI ZA AFYA

Mwenyekiti/Chairperson: Prof. Kaushik Ramaiya

Mkurugenzi Mtendaji na Daktari Mshauri katika Hospitali ya Shree Hindu Mandal – Dar Es Salaam na Katibu Mkuu wa Chama cha Kisukari Tanzania (TDA), Tanzania NCD Alliance (CEO & Consultant Physician at Shree Hindu Mandal Hospital & Hon. General Secretary of Tanzania Diabetes Association (TDA), Tanzania NCD Alliance (TANCDA)

Wasilisho: Huduma Jumuishi za Tiba Asili katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

Jina: Dr. Winifrida Benedict Kidima

Cheo: Kaimu Mkurugenzi Msaidizi, Kurugenzi ya Huduma za Tiba, Sehemu ya Tiba Asili na Mbadala

Taasisi: Wizara ya Afya

Barua pepe: winifridakidima@afya.go.tz

Utangulizi na Umuhimu: Zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania hutumia dawa za tiba asili kujitibu dhidi ya magonjwa mbalimbali. Wizara ya Afya inaendelea kuboresha huduma za tiba asili nchini kuendana na Sera ya Afya ya Mwaka 2017 na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Tano (2021/22-2025/26) unaosisitiza kuimarisha ujumuishwaji wa huduma za tiba asili zilizothibitishwa kisayansi kwa manufaa ya wananchi. Umuhimu wa huduma jumuishi za tiba asili umesisitizwa pia katika Mpango Mkakati wa Tiba Asili wa Shirika la Afya Duniani (2014-2025) katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote. Idara ya Tiba kupitia Sehemu ya Tiba Asili na Mbadala ilianzisha huduma jumuishi za tiba asili mnamo Mei 2023 kwa kuwajengea uwezo jumla ya watumishi 21 wa afya katika hospitali saba (7) za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Arusha, Tanga na Temeke-Dar es Salaam.

Malengo: Lengo la andiko hili ni kutathmini matokeo ya huduma jumuishi za tiba asili katika hospitali 7 za rufaa za Mikoa.

Mbinu na Taratibu zilizotumika: Tathimini hii imefanyika kwa kupitia taarifa na ripoti za utekelezaji wa huduma hizi kwa kila robo mwaka.

Matokeo: Matokeo yanaonyesha kwamba dawa aina 26 za tiba asili zilizokidhi vigezo vya usalama na ubora zimeatumika katika huduma hizi. Wastani wa wagonjwa 124 wametibiwa kwa kipindi cha kila robo mwaka na kufanya jumla ya wagonjwa waliotibiwa kufikia 868 tangu huduma hii ianzishwe mnamo Mei 2023 kufikia Machi 2025. Magonjwa ambayo yametibiwa ni pamoja na vidonda vya tumbo, pumu, mfumo wa upumuaji, homa ya matumbo, mvurugiko wa homoni kwa wanawake, maambukizi ya mfumo wa mkojo, bawasili, athritisi na tezi dume. Vilevile huduma hizi zimeingiza mapato ya jumla ya shilingi 26,118,529.

Hitimisho na Ushauri: Kutokana na hayo Serikali itaendeleza kuboresha huduma za tiba asili kwa kuchochea tafiti na ubunifu ili huduma za tiba asili ziwe na ubora, usalama na ufanisi.

Title: Integrative Health Services Using Traditional Medicine Services in Regional Referral Hospitals

Name: Dr. Winifrida Benedict Kidima

Position: Acting Assistant Director – Directorate of Curative Services, Traditional and Alternative Medicine Section

Institution: Ministry of Health

Email: winifridakidima@afya.go.tz

Background /Introduction and rationale: Over 60 percent of Tanzanians use traditional medicine to treat a wide range of illnesses either before or after consulting modern medical facilities for definitive treatment. The Ministry of Health (MoH) continues to promote traditional medicine services in the country in accordance with the 2017 Health Policy and the Fifth Health Sector Strategic Plan (2021/22-2025/26) that aims at enhancing the integration of evidence-based traditional and alternative medicine into health services for the public. The resolutions of World Health Assembly recognize the importance of traditional medicine and its integration into national health systems to enhance health and well-being worldwide in achieving Universal Health Coverage. Accordingly, in May 2023, the Department of Curative Services, Traditional and Alternative Medicine Section in the MoH introduced integrated health services using traditional medicine in seven Regional Referral Hospitals in Dodoma, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Arusha, Tanga, and Temeke-Dar es Salaam.

Objective(s): The purpose of this report is to evaluate and assess the outcomes of integrated health services in the seven referral hospitals.

Methodology/Approach: This assessment was carried out by analysing the quarterly implementation reports of the integrated health services.

Results: The findings show that 26 different types of natural remedies that met safety and quality standards were used in these services. From May 2023 to March 2025, the integrative health service served a total of 868 patients, with an average of 124 patients every three months. The ailments treated included peptic ulcers, asthma, upper respiratory infections, typhoid fever, hormonal imbalances in women, urinary tract infections, haemorrhoids, arthritis and benign prostate hypertrophy. These services have also resulted in a total revenue of 26,118,529 shillings.

Conclusions & Recommendations: Against this backdrop, the Government will continue to support traditional medicine services by promoting evidence-based services to ensure safety quality and efficacy.

Wasilisho: Mchango wa Huduma Jumuishi za Afya Ngazi ya Jamii katika Kuwezesha Huduma za Afya kwa Wote Nchini Tanzania

Jina: Norman Jonas Kyala

Cheo: Mratibu wa Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

Taasisi: Wizara ya Afya

Barua Pepe: Norman.kyala@afya.go.tz

Utangulizi na Umuhimu: Upatikanaji wa huduma ya afya kwa wote (UHC) unahitaji juhudi madhubuti kuhakikisha kila mtu anapata huduma bora za afya kwa usawa. Nchini Tanzania, afya ya jamii imekuwa mhimili muhimu wa huduma ya afya ya msingi (PHC) tangu utekelezaji wa sera ya ujamaa wa vijiji miaka ya 1960 na kampeni za afya miaka ya 1970. Hata hivyo, kwa miongo kadhaa, juhudi nyingi za afya ya jamii zilikuwa zimetawanyika, zenye mwelekeo wa magonjwa mahususi, na zikiendeshwa na wafadhili bila uratibu madhubuti. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara ya Afya ilizindua Mpango wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Ulio Sanifiwa na Kuratibiwa (ICCHW) mwaka 2024, ikiwa ni hatua ya kimkakati ya kuimarisha nafasi ya afya ya jamii katika kufanikisha UHC.

Malengo: Kuwasilisha mchango wa huduma za afya ya jamii katika kuimarisha UHC

Mbinu na Taratibu Zilizotumika: Huduma za Afya Ngazi ya Jamii imejengwa juu ya historia tajiri ya Tanzania katika afya ya jamii, kuanzia Azimio la Arusha la mwaka 1967, Mkutano wa Alma-Ata wa 1978, hadi kikao cha wadau cha Bagamoyo mwaka 2012. ICCHW inalenga kuajiri jumla ya CHWs 137,294, wawili (mwanamume na mwanamke) kwa kila Kitongoji na Mtaa. Wahudumu huchaguliwa na jamii kwa vigezo maalum, wakiwemo kuwa wakazi wa eneo husika, kuaminika, na kuwa na elimu ya sekondari. Mafunzo ya miezi sita yanayotolewa yanazingatia umahiri na yamejikita katika kuweesha CHW kutoa huduma za msingi za afya, lishe na ustawi wa jamii ndani ya jamii.

Matokeo: Mpango wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (CHW) umeleta mageuzi ya kimfumo katika utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania kwa kujenga mfumo jumuishi, unaoratibiwa kitaifa na kuzingatia usawa wa kijinsia, kijamii na kijiografia. Mageuzi haya yamehakikisha kuwa huduma za afya ngazi ya jamii si tu sehemu ya huduma ya afya ya msingi bali pia ni chombo muhimu cha kufanikisha huduma ya afya kwa wote (UHC). Kupitia mpango huu, CHWs wanaunganishwa rasmi katika mfumo wa afya wa taifa kupitia sera, taratibu za usimamizi, ufuatiliaji wa kimkakati na matumizi ya mifumo ya kidijitali kama DHIS2.

Uteuzi wa CHWs unatekelezwa kwa kushirikisha jamii kwa kutumia vigezo vilivyo wazi na vinavyozingatia usawa na uadilifu. Mtu anapaswa kuwa na elimu ya angalau kidato cha nne, awe mkazi wa kudumu wa mtaa au kitongoji husika kwa angalau miaka mitatu, awe na sifa za kuaminika kijamii, asiwe na historia ya makosa ya jinai, na awe na utayari wa kutoa huduma kwa kipindi kisichopungua miaka mitano. Baada ya uteuzi, CHWs hupata mafunzo ya miezi sita yaliyo boreshwa kwa msingi wa umahiri katika maeneo saba ya kipaumbele: elimu ya afya na uhamasishaji, afya ya uzazi na watoto, magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, lishe na udumavu, ustawi wa jamii, usafi wa mazingira, na magonjwa mapya. Lengo ni kuwajengea uwezo wa kutoa huduma jumuishi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wanayoihudumia.

Ugawaji wa CHWs unafanyika kwa uwiano wa jinsia, ambapo wawili (mmoja mwanamume na mmoja mwanamke) wanapangwa kwa kila Kitongoji au Mtaa. Kwa jumla, nchi inahitaji wahudumu 137,294 ili kufikia maeneo yote 64,384 ya vijijini na 4,263 ya mijini. Wakiwa sehemu ya mfumo rasmi wa afya, CHWs hutoa huduma jumuishi zinazogusa maeneo yote ya mnyororo wa huduma: kuhamasisha (mfano: chanjo, lishe, elimu ya afya), kinga (mfano: utoaji wa vyandarua, uchunguzi wa shinikizo la damu na kisukari), tiba ya msingi (mfano: matibabu ya malaria na kuhara).

Mpango huu shirikishi umeongeza ufanikishaji wa upatikanaji wa huduma bora, usawa wa kiafya, na uthabiti wa mfumo wa afya unaomfikia kila mwananchi moja kwa moja hadi ngazi ya kaya.

Hitimisho na Ushauri: Mpango wa ICCHW ni hatua ya kimkakati kuelekea huduma jumuishi, zinazomlenga mtu na zinazoongozwa na jamii. Kwa kuwaweka CHWs ndani ya mfumo rasmi kwa kutumia sera, rasilimali na mifumo ya taarifa za kidijitali, Tanzania inaondoa changamoto za kihistoria na kuweka mfano bora kwa nchi nyingine zenye kipato cha chini na cha kati. Wigo wa huduma unaoendana na nguzo kuu za UHC: upatikanaji, usawa, ubora, na uendelevu wa huduma kwa wote.

Title: *The Role of Integrated Community-Based Health Services in Advancing Universal Health Coverage in Tanzania*

Name: Norman Jonas Kyala

Position: Coordinator of National Community Based Health Services

Institution: Ministry of Health

Email: Norman.kyala@afya.go.tz

Introduction and Rationale: *Achieving Universal Health Coverage (UHC) requires deliberate efforts to ensure equitable access to quality health services for all. In Tanzania, community health has been a pillar of primary health care (PHC) since the implementation of villagization policies in the 1960s and national health campaigns in the 1970s. However, for decades, most community health efforts were fragmented, disease-specific, and donor-driven with minimal coordination. To address these challenges, the Ministry of Health launched the Integrated and Coordinated Community Health Worker (ICCHW) Program in 2024 as a strategic step to strengthen community health in achieving UHC.*

Objective: *To present the contribution of community health services in advancing UHC.*

Methodology/Approach: *Tanzania's community health system builds on a rich legacy, from the 1967 Arusha Declaration and the 1978 Alma-Ata Conference to the 2012 Bagamoyo Stakeholder Meeting. The ICCHW Program targets recruitment of 137,294 CHWs—two (one male, one female) per Kitongoji or Mtaa. CHWs are selected by the community based on clear criteria, including local residency, trustworthiness, and secondary education. They undergo six months of competency-based training designed to equip them with practical skills in primary health care, nutrition, and social welfare.*

Results: *The ICCHW Program has brought systemic reforms by creating an integrated, nationally coordinated structure that considers gender, social, and geographical equity. CHWs are formally embedded within the health system through supportive policies, supervision structures, strategic monitoring, and digital systems like DHIS2. The selection process ensures social acceptance and accountability. Training covers seven priority modules: health promotion, RMNCAH, infectious and non-communicable diseases, nutrition, social welfare, environmental health, and emerging diseases. With equitable deployment (two CHWs per hamlet/urban cell), Tanzania aims to serve all 64,384 rural hamlets and 4,263 urban Mitaa. CHWs provide*

promotive (e.g., immunization and health education), preventive (e.g., blood pressure screening), basic curative (e.g., malaria and diarrhoea treatment), rehabilitative, and palliative services. The inclusive model increases service coverage, health equity, and community-level resilience cornerstones of UHC.

Conclusion and Recommendations: *The ICCHW Program is a strategic step toward people-centered and community-driven integrated health services. By embedding CHWs into the formal health system through strong policy, financing, and digital monitoring, Tanzania is overcoming historical inefficiencies and offering a replicable model for other low- and middle-income countries. The wide scope of community-delivered services aligns directly with the pillars of UHC: availability, equity, quality, and sustainability for all.*

Wasilisho: Utafiti wa ufuatiliaji wa Viashiria hatarishi na tathmini ya Hali ya Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (STEPS Survey)

Jina: ¹Mary T. Mayige & ²Omary Ubuguyu on behalf of the STEPS Survey Technical Committee

Cheo: ¹Mtafiti Mkuu na Mkurugenzi wa Taarifa za Utafiti na Kurekebu Tafiti & ²Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Magonjwa Yasiyoambukiza na Afya ya Akili

Taasisi: ¹Taasisi ya Tafiti ya Magonjwa ya Binadamu – NIMR & ²Wizara ya Afya

Barua pepe: maryma13@yahoo.com & oubuguyu@gmail.com

Utangulizi: Ukubwa wa tatizo la magonjwa yasiyoambukiza (MYA) unaendelea kuwa tatizo la msingi la afya ya Jamii nchini, ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa madhara na vifo vitokanavyo na magonjwa haya. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa ufuatiliaji wa viashiria hatarishi na tathmini ya hali ya magonjwa yasiyoambukiza nchini (STEPS Survey) kwa mwaka 2011 Zanzibar na mwaka 2012 kwa Tanzania Bara inaonesha MYA na viashiria vyake vipo kwa kiasi kikubwa. Ripoti hii itaelezea utafiti ulivyofanyika na matokeo ya utafiti kwa mwaka 2023.

Malengo: Utafiti umefanyika ili kuwezesha kupata takwimu za kitaifa za viashiria hatarishi vya Magonjwa yasiyoambukiza kwa Tanzania kwa ujumla, Tanzania Bara na Zanzibar.

Njia Zilizotumika (Methods): Huu ni utafiti wa majumbani uliohusisha kaya ambapo sampuli ilipatikana kutokana na vigezo vilivyozingatia mgawanyo katika hatua za makundi matatu. Walengwa walikuwa watu wote kwenye jamii waliokuwa na umri wa miaka 18 hadi 69 ambao wakati wa utafiti katika kaya zilizoteuliwa walitambuliwa kama wakazi wa kaya hizo. Taarifa za Sensa ya watu na makazi za mwaka 2022 zilitumika kutengenezea mwongozo wa utambuzi wa kaya kwa ajili ya Utafiti huu (STEPS Survey 2022/23). Jumla ya watu 4,320 walishiriki utafiti huu kwa mgawanyo wa washiriki 3,780 kwa Tanzania Bara na washiriki 540 kwa Zanzibar. Takwimu zilikusanywa kubainisha viashiria hatarishi ambavyo vinajumuisha hali ya tabiabwe, ulaji usiofaa, matumizi ya tunbaku, pombe na hali ya sonona pamoja na masuala ya unene na uzito uliokithiri kwa kutumia mifumo rasmi na mbinu kutokana na miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO STEPS). *methodology.* Takwimu zilikusanywa kwa kutumia mfumo wa kieletroniki wa Open Data Kit (ODK) eSTEPS software. Utafiti ulifanyika kuanzia mwezi Septemba 2022 hadi Septemba 2023.

Matokeo: makadirio ya matokeo ya hali ya magonjwa yasiyoambukiza na viashiria hatarishi yatawasilishwa.

Hitimisho: Utafiti umebainisha ukubwa wa tatizo la shinikizo la damu, kisukari, hali ya changamoto za afya ya akili, sonona, ajali za barabarani, ajali ambazo hazikuhusisha ajali za barabarani pamoja na ukubwa wa vihatarishi vya magonjwa ya moyo. Utambuzi wa viashiria hatarishi umezingatia upimaji wa tabia au hali ambazo zinaweza kuchochea uwezekano mtu kupata magonjwa yasiyoambukiza. Uchambuzi wa hivi viashiria hatarishi utasaidia kutambua makundi ya kijamii yaliyo kwenye uhatarishi mkubwa na hivyo kubainisha mbinu za kuzuia magonjwa haya.

Title: STEPS Survey of non-communicable diseases, mental health, oral health and injuries in Tanzania

Names: ¹Mary T. Mayige & ²Omary Ubuguyu on behalf of the STEPS Survey Technical Committee

Position: ¹Principal Research Officer and Director of Research Information and Regulatory Affairs & ²Assistant Director of Non-Communicable Disease

Institutions: ¹National Institute for Medical Research & ²Ministry of Health

